# Kugeuza taka za samaki kuwa mbolea

Rutuba ya udongo ni jambo muhimu ambalo huamua tija ya ardhi, na inaweza kuboreshwa kwa kutumia mbinu sahihi za kilimo. Utumiaji mwingi wa mbolea za kemikali huharibu afya ya udongo, jambo ambalo hupungunza tija yake, na hilo linaweza kuboreshwa kwa kutumia nyenzo asili. Takataka za samaki ni sehemu za samaki ambazo watu hawali, na hizi zimekithiri Nitrojeni, fosforasi, kalsiamu na vitamini..

## Kutengeneza wa mbolea

Ili kutengeneza mbolea ya maji ya samaki, chachusha taka za samaki kwanza.Kata taka za samaki katika vipande vidogo ili kuharakisha uchachushaji na vaa glavu ili kuepuka majeraha. Viumbe hai ambavyo huchachusha taka huhitaji sukari kukua, kwa hivyo ongeza kilo 3 za sukari au molasi na uchanganye vizuri.
Vile vile, weka mchanganyiko huo kwenye ndoo ya plastiki, uifunike kwa kifuniko kisichopitisha hewa na uiweke kwenye kivuli. Kisha koroga mchanganyiko mara moja kwa siku na, mchanganyiko utakuwa tayari baada ya wiki 4. Chuja mchanganyiko kwa kitambaa cha pamba, na uweke mchanganyiko mahali pa giza.
Ili kutumia mbolea ya maji, yeyusha kwanza na kunyunyizia kwa mboga za majani na nafaka. Changanya lita 10 ya maji na lita 1 ya mbolea. Nyunyizia mimea mara mbili, yaani, wakati mmea ukiwa mchanga na wakati wa kutoa maua. Kwa mazao ya miti, changanya lita 2 za mbolea na lita 10 za maji na nyunyizia mmea wakati wa kuchanua maua na baada ya kuvuna.
Ili kutengeneza mbolea ya samaki ya udongo, chimba shimo la kina cha nusu mita na ukubwa kadhaa kulingana na wingi wa mbolea inayohitajika. Shimo lazima lichimbwe chini ya kivuli. Kata taka katika vipande vidogo, vichanganye na kilo 5 za sukari na ongeza kilo 65 za samadi ya ng’ombe iliyooza vizuri. Hamisha mchanganyiko kwenye shimo na lifunike na majani mapana hadi kina cha 1cm, mbolea itakuwa tayari baada ya miezi 2.
Baada ya kulima mara ya mwisho, weka kilo 20 za mbolea hii

iliyochanganywa na kilo 10 za samadi ya ng’ombe juu ya udongo. Hatimaye, weka mbolea kwenye mimea na miti mara moja baada ya kila baada ya miezi 3.